

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

680

UALIMU ELIMU YA AWALI

Muda: Saa 3

Jumanne, 05 Mei 2015 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali mawili (2) kutoka kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama 40, sehemu B na C kila moja ina alama 30.
4. Simu za mkononi haziruhusiwi katika chumba cha mtihani.
5. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu cha 1 o cha kujibia.

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. (a) Eleza kwa kifupi maana ya elimu jumuishi.
(b) Orodhesha changamoto tatu zinazotokana na utekelezaji wa elimu jumuishi.
2. (a) Tofautisha kati ya motisha shauku na motisha kishawishi.
(b) Bainisha matumizi mawili ya motisha kwa darasa la elimu ya awali.
3. Eleza kwa kifupi misingi minne ya ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya awali.
4. Fafanua kwa kifupi sifa nne za zana za kufundishia na kujifunzia watoto wa elimu ya awali.
5. (a) Eleza maana ya mtaala.
(b) Kwa kutumia hoja tatu, bainisha umuhimu wa mtaala katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji.
6. Tofautisha istilahi zifuatazo:
(a) Nukuu za somo na shajara ya somo.
(b) Tathmini ya somo na maoni ya somo.
7. Utoto uchanga huambatana na mabadiliko mengi katika ukuaji wa mtoto. Orodhesha mabadiliko manne yanayojitokeza katika kipindi cha utoto uchanga.
8. Eleza kwa kifupi historia ya mifumo ifuatayo ya elimu ya awali:
(a) Shule za kindergarten
(b) Montessori
(c) Shule za nursery
(d) Vituo vya kulea watoto wadogo.

9. Mwalimu Julius K. Nyerere (1922 – 1999) alikuwa mwanaelimu wa Kitanzania aliyekazia sana kuwa elimu ni haki ya msingi ya mtoto. Orodhesha mambo manne aliyoamini kuhusu elimu ya watoto wadogo.
10. Kwa kutumia hoja nne, fafania kwa kifupi utaratibu unaofaa kufuatwa ili kujaribisha zana za utafiti wa kielimu.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka katika sehemu hii.

11. Eleza dhana ya upimaji wa maendeleo ya mtoto wa elimu ya awali kisha bainisha zana sita zinazotumika katika upimaji wa maendeleo ya mtoto.
12. Tofautisha kati ya tathmini tatuzi na tathmini endelevi kisha eleza bayana matumizi sita ya taarifa za tathmini ya elimu ya awali kwa mwalimu, mzazi na mamlaka za elimu.
13. Eleza dhana ya uongozi wa elimu ya awali na majukumu sita ya kamati ya shule ya awali.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka katika sehemu hii.

14. Hadithi ni mojawapo ya njia za kufundishia zilizomo katika kundi la njia za maelezo. Fafania hatua sita ambazo mwalimu anapaswa kufuata endapo anataka kufundisha kwa kutumia hadithi au simulizi.
15. Andaa somo la vitendo vya kujifunzia hisabati kwa darasa lenye watoto 28 kwa lengo la kufundisha mada ndogo "msamiati wa namba."
16. Elezea vigezo vitano vya kuzingatia katika kuchagua mbinu za kufundishia na kujifunzia elimu ya awali.